

WALINZI WA MAZINGIRA

TOLEO LA 1

*Ulinzi wa mazingira yetu
ni jukumu letu*



Hadithi ya Salima na mapambano ya mabadiliko tabia nchi

**Salima na mapambano ya mabadiliko tabia nchi
Walenzi wa Mazingira**

Salima na rafiki yake Amani wanagundua jinsi plastiki inavyoathiri mazingira yao na kuchangia katika mabadiliko ya hali ya tabia nchi yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu tunazoziona kila siku. Salima anachukua hatua ya kuungana na Amani kwa vita dhidi ya nguvu za uovu zinazozuia jamii kuona na kupingana na athari za mabadiliko ya tabia nchi yanayoletwa na jitu lisiloonekana linaloitwa Magugu. Fungua kurasa za ndani ya hadithi hii ya michoro kuona jinsi vijana wanaweza kuchukua hatua ya kuhamasisha jamii kulinda mazingira yao.

Washiriki waandaaji: WeWorld na Hakuna Matata
Watayarishaji: Tai Plus Co. Ltd
S.L.P 54631
Kinondoni, Dar es Salaam
business@taiplus.co.tz
Tel: +225766748888

Mwandaaji na Muongozaji: Gwamaka Mwabuka
Mchoraji: Yohana Mwenda
Mwandishi: Padili James
Msanifu: Samli Salum

Washiriki kutoka WeWorld

Piero Meda *Mkurugenzi Mkaazi*
Winifrida Kaheshi *Mkurugenzi Msaidizi na Meneja Ufuatiliaji na Tathmini*
Francesco Paris *Meneja wa Mradi Kijani Pemba*
Moh'd Rashid *Mratibu wa Utekeleza Mradi Kijani Pemba*
Shaibu Hussein *Afisa Ufuatiliaji na Tathmini/Meneja Msaidizi wa Elimu*
Jacquiline Olotu *Afisa Maendeleo ya Jamii*
Agnes Victor *Meneja Mashirikiano na Taasisi/ Afisa Ufuatiliaji na Tathmini*

Mshiriki kutoka Hakuna Matata

Azzurra Cori *Director*

Kuhusu WeWorld:

WeWorld ni shirika huru lisilokuwa la kiserikali linalofanya kazi za maendeleo na misaada ya kibinadamu kwa kushirikiana na jamii na mamlaka husika kwa zaidi ya miaka 50, kwasasa linafanya kazi katika nchi 27. Shirika linafanya kazi Tanzania tokea 2010. Walengwa na wahusika wakuu ni watoto, wanawake na vijana, pamoja na wapenda mabadiriko chanya kwa kila jamii katika nyanja zifuatazo: haki za binadamu (usawa wa kijinsia, kuzuia unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto na wahamiaji), misaada ya kibinadamu (kuzuia unyanyasaji, kutoa misaada na huduma kisaikolojia), usalama wa chakula, maji na usafi wa mazingira, afya, elimu na ujifunzaji, maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ulenzi wa mazingira, elimu ya uraia duniani na kujitolea kimataifa.



KATIKA MJI WA MAKUTANO, JITU LIMEINGIA, LINALOTISHA WATOTO NA KUFURAHIA UHARIBIFU WA MAZINGIRA UNAOFANYWA NA WATU WAZIMA.



NYUMA YA PORI LA MZEE KASANDA !!!
NYUMA YA PORI LA MZEE KASANDA !!!



MSITU WA MAPENDO 10:30 JIONI



MHHH! MBONA...
MIMEA ALIYONITUMA
BIBI IMEHARIBIWA.

NGOJA NIONGEE
NAO KWANINI
WAMEKATA
DAWA ZA BIBI.



KWANINI
MMEKATA MITI,
MMEHARIBU
DAWA ZA BIBI
YANGU. MSIKATE
MITI JAMANI

SHIKAMOO!

MARAHABA




WEWE MTOTO
HEBU RUDI
NYUMBANI USIJE
ANGUKIWA NA
MTI UKATUPA KESI,
NENDA!

BIBI SI
ATATESEKA
SANA BILA
MITISHAMBA
YAKE,
NITAMWAMBIA
NINI LEO
JAMANI.



BAADA YA MAMA YAKE KUFARIKI KWA KIPINDU PINDU, SALIMA ALIISHI NA BABA NA BIBI YAKE.



WAMEKATA MITI KOTE KULE
KWA MZEE KASANDA.
NIMEPATA HII TU.


TUMEKWISHA. KAMA HALI NI HII,
HATUNA CHETU TENA, TUTAKUFA
WATU HAWANA ADABU NA MITI.
NITAPATA WAPI DAWA
ZANGU SALIMA?

USIJALI BIBI, NITAFUATILIA
ZAIDI KESHO, IKIBIDI KUIPANDA
HAPA TENA NIONE KAMA
ITAOTA.



NGAAA
NGAAA
NGAAA!
KWANG!

UCHAFUZI WA MAZINGIRA ULISABABISHA
KUZUKA KWA MAGONJWA YA MLIPIKO
KILA MARA.



**HAAAAHAHA!
SAFI SANA!
CHAFUAA.**

VYANZO VYA MAJI VILICHAFULIWA HASA MTO
KIRRASA.




MEEE!

TUONGEZE ZINGINE BOSI.

ACHA UOGA. KIBALI CHA
KUBEBA UNACHO.

BABA SALIMA ALIKUWA MLIUZA MBOAO
MAARUFU MWENYE UCHU WA PESA.



AAAAH, HAPANA ZIMETOSHA,

MZEE, ZIMETOSHA
ACHA TAMAA.

SALIMA ALISOMA SHULE YA MSINGI MAKUTANO, DARASA LA SITA B. ALIKUWA KIRANJA WA USAFI NA MWENYEKITI WA KLABU YA MAZINGIRA.



SALIMA ALIKUWA MWANAFUNZI MWEREVU, ALIYEPENDWA NA WALIMU HASA MWALIMU YASINTA AMBAYE NI MWENYEKITI WA KAMATI YA USTAWI WA KIJIKI.



ATAKAYE PATA KUENZIA KUMI NA NANE, NAMRUHUSU KUONDOKA MAPEMA.

SALIMA UGANIPA LIFT LEO.

LEO NAENDA MSITUNI KUMTAFUTIA BIBI DAWA ZAKE.

SALIMA HAKOSI.

KAMA KAWAIDA, SALIMA, ISHIRINI YA ISHIRINI, WAHI NYUMBANI KAMSAIDIE BIBI KAZI. USISAHAU MICHE YA KLABU KESHO.



SAWA. AHSANTE MWALIMU, KWAHERI.

MWANAMAZINGIRA LEO KALUPEGA MWINGI.

TULIA DOGO, ACHA KUMWONEA MWENZIO GERE.



LIKATAJI MITI ULIONDOA HISTORIA NDEFU YA UTOTO WA SALIMA.




WAMEKATA YOTE.


WATOTO WENGINE WALIPENDA KADOME, KOMBOLELA NA MPIRA, SALIMA ALIPENDA MISITU.



GHAFLA MAGUGU LIKAMTOKEA SALIMA, KUMTISHA SABABU LILIKUWA LINAOGOPA WATOTO WEREVI



**BIBI SALIMA ALIMFUNZA MJKUUU WAKE
KUTUNZA BUSTANI NA HADITHI ZA KALE**



SI KAMA VUMBI VUMBI?

NDIO BIBI, NDIO LINAITWA MAGUGU
KUMBE LINAONGEA KAMA MTU,
KAMA ULIVYONISIMULIA KWENYE
HADITHI NILIPOKUWA LA NNE.

NI ISHARA YA KUKITHIRI KWA
MABADILIKO TABIA
NCHI KIJIJINI
KWETU.

ITABIDI TUFANYE KITU
BIBI, SITAKI KUONA
MITI IKIHARIBIWA.



SASA MAMA TUTAPATA
WAPI PESA??

ILA MUACHE KUKATA MITI,
MNAHARIBU MITISHAMBA
YETU JAMANI.

BABA UNaweza KUTENGENEZA
BIDHAA ZA CHUMA KAMA MAJIKO
SANIFU NA KUPUNGUZA UKATAJI
WA MITI

MH! WAZO LAKO
NITALIFIKIRIA



HATA KAMA MAGUGU
ANATISHA SITAKI
AHARIBU MAZINGIRA,
NITAFANYAJE SASA?

HATA MIMI NILIWAHI SIKIA HILO
JITU MAGUGU, LINAWATOKEA
WATOTO WAKOROFI, SIJUI
WACHAFU...

WE SALIMA
LINAUHAKIKA,
HUOGOPI?



AMANI ALIKUWA RAFIKI KIPENZI WA SALIMA.

BIBI KASEMA NI ISHARA YA KESHO
YETU KUIBIWA NA WATU WAZIMA
WASIOHESHIMU MAZINGIRA.
SIJUI NI KWELI.

NDIO, PIA BIBI HUSEMA HUTAKIWI
KUOGOPA UNAPOYALINDA MAZINGIRA
YAKO. LEO TWENDE
TUONE KAMA KWELI.



LAKINI TUNAFANYA USAFI,
TUNAKUSANYA TAKA NA KUZITUPA
MAHALI SAHIHI.

YOTE NI SAWA, ILA KUNA GHARAMA
YA KUSAFIRISHA MPAKA DAMPO,
ONA TAKA ZINAVYO HARIBU MTO

SALIMA ALIRITHI ROHO YA UJASIRI YA BABA YAKE, HAKUOGOPA VITISHO VYA MAGUGU.



SIJUI YLIKO WAPI, ILA NILIPOPATA WAZO TU LA KUCHUMA MIMEA NIKAPANDE NYUMBANI LIKATOKEA KUNITISHA.

LIKITOKEA MIMI NALIPIGA FIRE MOJA HATARI NILIJIFUNZA KANISANI.



NIMEWASIKIA NYIE WANAMAZINGIRA MKIPANGA KUNIHARIBU, HAYA SASA TUZUNGUMZE.



MIMI NI ZAO LA UCHAFUZI MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI YATOKANAYO NA SHUGHULI ZA BINADAMU. NYIE VITOTO MNADHANI MTANIWEZA?

SIKLOSOPI NA NIMEKUJA KUKWAMBIA NITAWAHAMASISHA WANAFUNZI WENZANGU TURUDISHE MITI, PUNGUZA MATUMIZI YA BIDHAA ZA PLASTIKI, KAMA KUTUMIA CHUPA MOJA YA MAJI, KAMA MIMI.

TUTaweza.

NA KUTUMIA KIKAPU KWA MANUNUZI, BADALA YA MIFUKO YA PLASTIKI NA KUTUMIA CHUPA MAALUM ZA MAJI KWA MATUMIZI YA KILA SIKU.

MASWALI


1. KIJIKI CHAO SALIMA KINAKUMBWA NA KITU GANI KINACHOBADILISHA TABIA NCHI?
2. NI SHUGHULI GANI ZINAZOFANYWA NA WANAKIJIKI WA MAKUTANO ZINAZOHARIBU UOTO ASILI NA KUBADILI TABIA NCHI? ZITAJE?
3. MAGUGU NI JITU LINALOWAKILISHA AMA KUMAANISHA KITU GANI KINACHOTOKEA KIJIKINI KWAO SALIMA?
4. JE? WEWE UNATUNZA MAZINGIRA? KAMA UNATUNZA, TUAMBIE UNATUMIA NJIA GANI KUYATUNZA MAZINGIRA YA MTAANI KWENU AU NYUMBANI?



BAADA YA KUTAMBIANA NA SALIMA, MAGUGU ALILETA
MAFURIKO NA PEPO KALI, NDANI YA WIKI TATU.



WANAFUNZI WOTE, WALIBAKI DARASANI
MPAKA MVUA ILIPOKATIKA NA HALI KUWA
SHWARI.



MAGUGU ALISEMA ATAONYESHA
MOJA YA ATHARI ZA KUJARIBU
MAZINGIRA YETU, HII SI
MOJA WAPO.

NDIO, MVUA ZISIZOTABIRIKA
NA MAFURIKO NI MOJA
YA ATHARI ZA MABADILIKO
YA TABIA NCHI.



JAMANI ONA MAFURIKO YALIVYO HARIBU,
BUSTANI YANGU SIJUI ITAKUWA IMEPONA?

ONA ATHARI ZA MABADILIKO
YA TABIA NCHI ZILIVYONIHARIBIA
BUSTANI YANGU BIBI.

POLE MJUKUU WANGU,
KHEE, MTAMA WANGU
UTAKUWA UMEBAKI
KWELI KULE SHAMBANI?

NITAENDA
KUKUANGALIZIA
BIBI USIJALI



MASHAMBA YA MTAMA.

MUNGU WANGU
MASHAMBA YOTE
YAMEHARIBIKA,
BIBI ATAUMIA
SANA, AMANI ONAA.

SALIMA ITABIDI
TWENDE TUKAWAAMBIE
WAZAZI KUHUSU
MAGUGU ILI TUSIPITIE
MADHARA MENGINE.



TUMWAMBIE BABA,
MWALIMU YASINTA ILI
WASHIRIKIANE KUWAAMBIA
WACHAFUZI WAACHE.

MMEONA ATHARI
ZANGU. NA HII
NI TRELA.





MMEONA UKATAJI MITI, UCHOMAJI MKAU UNAVYONIPA NGUVU ZA KULETA MAAFA. SI NILIWAAMBIA WAKUBWA NI WAHARIBIFU MKAKATAA.

MNANISINGIZIA BURE, MIMI SINA NGUVU BILA NYIE KUHARIBU MAZINGIRA, KWAHERI.

TUSAMEHE, USILETE ATHARI ZINGINE, TUTAWAAMBIA WAACHE KUHARIBU MAZINGIRA.

MAFURIKO YAKO YAMEHARIBU BUSTANI YANGU NA MTAMA WA BIBI.

MAGUGU LITAONDOKA KIJIKI KWETU. SUBIRI NIWAHAMASISHE WENZANGU WAANZE KUPUNGUZA MATUMIZI YA CHUPA NA BIDHAA ZA PLASTIKI ZA MATUMIZI YA MARA MOJA.

LIONE, KWANZA LIJITU LENYEWE LIBAYA.

KWA HIYO BIBI, ITABIDI TUTUNZE HELA KWENYE KIBUBU, KWAAJILI YA JIKO SANIFU AU GESI, TUOKOE MITI NA MAZINGIRA, PIA KUNA NJIA ZINGINE.



ENHE, ZIPI HIZO?

OOH VIZURI, SASA MWANAMAZINGIRA MZURI, HUANZA NYUMBANI. UTATUMIA VIPI ULICHOJIFUNZA?

NI, KUPUNGUZA, MATUMIZI YA PLASTIKI NA KUTUMIA VIKAPU AU CHUPA MOJA TU YA MAJI. KUTUMIA TENA NA KUCHAKATA TENA BIDHAA TUNAZOTUMIA KILA SIKU.

SALIMA ALIPUNGUZA MANUNUZI YA PLASTIKI KWA VITENDO.




VITU VYOTE MNAVYOVITAKA VIKO KATIKA PAKITI ZA PLASTIKI. SI MNUNUE TU KWANI VINATATIZO GANI?

HAPANA, VINA MADHARA KATIKA MAZINGIRA MAANA VIMEFUNGASHWA NA PLASTIKI.



MMH, UANA MAZINGIRA HUU. HAYA.

SITAKI KUCHAFUA MAZINGIRA NA PLASTIKI. NDIO MAANA NABEBA VIFUNGASHIO VYANGU SALAMA.





BAADAE, JIONI.

SALIMA ALIISHI ALICHO KISEMA. ALIKUWA NA CHUPA MAALUM YA MAJI, ALIYOKUWA AKITUMIA KILA SIKU NA KUEPUKA MATUMIZI YA CHUPA ZA PLASTIKI.



SALIMA ALIKUWA KIONGOZI WA KLABU YA MAZINGIRA NA KILA JUMATANO, ALIENDESHA SHUGHULI ZA KLABU NA AMANI.



SALIMA ALIJIWEKA HATARINI KULINDA MISITU KWA KUKABILIANA NA WAKATAJI MITI WAKOROFI.




WEWE DOGO HEBU TOKA HAPA USIJE TULETEA KESI.

SEPA KULE. UTUNZAJI MAZINGIRA BONGO!.

SITAKI, MNAHARIBU MAZINGIRA. MNAMPA NGUVU MAGUGU.

MDOGO WANGU HEBU NISIKILIZE BASI, RUDI SHULE KWANZA, UTARUDI BAADAE.



MAGUGU NDIO NANI TENA?

NI JITU LINALO WAKILISHA ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIA NCHI.

JINI AU POPO BAWA? HAHA, DOGO UMECHANGANYIKIWA.



ACHA! UNAHARIBU MAZINGIRA.

NYIE WACHAFUZI HAMUWEZI MWONA KWAVILE, SIO KESHO YENU MNAYOIHARIBU. SISI WATOTO NDIO TUKAKAO JUTA PALE MVUA, MIMEA NA MAJI YAKIPOTEA. WEWE USIKATE MTI...



WEWE MTOTO USHAANZA LETA MAZOEAE. UNALINDA MTI WA KWAKO, TOKAA HAPA.


NISIKILIZENI, MNAHARIBU UOTO, KWA VILE MMEKATA SANA BILA KUPANDA, WALA KUFUATILIA MWENENDO WA TABIA NCHI.



MAMAAAA!

MASWALI

1. KWANINI NI VIBAYA KUKATA MITI KIHOLELA BILA KUPANDAALI KUFUATILIA TAARIFA YA UOTO ASILI YA MSITU AU ENEO?
2. JEP NJIA ALIYOTUMIA SALIMA KUKABILIA NA UKATAJI MTI NI SAHIHI?
3. NI NJIA GANI AU MBINU NZURI, UNATAKIWA KUIFANYA KUKABILIANA NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA.
4. NI NJIA GANI HUTUMIKA SHULENI KWENU KUTUNZA MAZINGIRA NA KUJIFUNZA KUHUSU MABADILIKO YA TABIA NCHI NA MAZINGIRA?



BAADA YA KUFUKUZWA NA WAKATA MITI, SALIMA HAKUKATA TAMAA NA KWENDA KWA WACHOMA MKAA.



BINTI RUDI SHULE,
USILETE MCHEZO NA SISI.
HAYA MAMBO YA WAKUBWA.
MAZINGIRA HUYAJUI WEWE.

KWA HIYO WEWE
NDIO UMEKUJA
KUTUFUNDISHA
USAFI, SISI
WACHAFU
SIO.

BAADA YA KUSHINDWA HAMASISHA WAKATA MKAA ALIRUDI NYUMBANI NA KUBADILI NGUO NA KUENDELEA NA HATU YA TATU, SOKONI.




SISI WATOTO NDIO
TUTAKAOJUTA
MBELENI NA MADHARA YA
MABADILIKO YA TABIA NCHI.

SI MTOTO WA
GAMBI
HUYU, LINI KAAZNA
UTUNDU?.

NENDA KALALE, UMECHOKA
WEWE MTOTO.

ACHA KELELE
WE BINTI.



BABA YAKO ANAJUA
UMEKUWA HUNA
ADABU SIKU
HIZI?

KEI, KEI IPI
HIYO.

HAPANA, SHULENI
TUMEFUNDISHWA
MADHARA
YA KUTOTUNZA
MAZINGIRA
NA KUTOFUATA
K TATU.

KUPLUNGIZA,
KUCHAKATA
TENA NA
KUTUMIA
BIDHAA
ILI KUTOTUPA
TAKA.

TOKA HAPA NA
KEI ZAKO.



NAKIONYA ACHA TABIA
ZA KUSUMBWA WAKUBWA
NA SAYANSI ZAKO ZA UONGO NA KWELI.
ETI MAFURIKO, NJAA NA MAZAO
KUFA, MAGONJWA YA MLIPIKO YATAKUJA
MSIPO TILIA MAANANI KANUNI ZA
MAZINGIRA. WEWE!!!

NI KWELI BABA,
TUMEFUNDISHWA
SHULE NANIMELIONA
JITU LA...

NYAMAZA!




KWANINI BABA NA
WATU WAZIMA
WENGI HAWATUSIKILIZI
WATOTO?

BAADA YA MIEZI KUMI NA SABA.



MJI WA MAKUTANO ULIKUMBWA NA UKAME MKALI, ULIOKAUSA MTO, MAZAO, UA MIFUGO NA KUUFANYA MJI KUKOSA MAJI NA CHAKULA MPAKA KUOMBA MSAADA TOKA SERIKALINI.

SERIKALI ILIINGILIA KATI NA KUZUIA UVUNAJI MITI KIHOLELA, BAADA YA MWALIMU YASINTA KUTOA MALALAMIKO KUPITIA BARUA MAALUM.



MAMLAKA YA WILAYA, ILIANZA TAFUTA MBINU MBADALA KULETA MSAADA NDANI YA MAKUTANO ILI KUWAOKOA WANAKIJIJI.



JAMANI MAJI YATOKA PALESTINA JAMANI CHANGAMKENI HUKO.

WENGINE HATUJAOGA MWEZI WA PILI SASA.



Hahaha. ENDELEA MIMI SINA SHAKA. NAFURAHIA KUONA KESHO YAKO SI YA KIJANI TENA.

NIMEKUJA KUKWAMBIA, HUJASHINDA BADO. VITA DHIDI YA UCHAFUZI NA MABADILIKO YA TABIA NCHI INAENDELEA NA MUDA SI MREFU KIJANI KITARUDI TENA.

MASWALI

1. JEP? SALIMA ALITUMIA NJIA BORA KUHAMASISHA WANAKIJIJI WENZAKE?
2. NI NJIA GANI UNGETUMIA KUWASHAURI WATU WANAOFUUA Mazingira na kutotilia maanani mazingira?
3. JEP? UNADHANI WATU WAZIMA NA WATOTO WANaweza unghana na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi?
4. NI ATHARI GANI ZAIDI ZINAZOWEZA IKUMBA JAMII INAYOKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI?



SALIMA HAKUKATA TAMAA. ALIKUJA NA MPANGO MPYA, ULIOPEWA NGUVU NA MARAFIKI NA MWALIMU YASINTA.



HAYA SALIMA TUANZE KAZI YA KUHAMASISHA MABADILIKO.




MLIMDHARAU SALIMA ALIPOWAONYA NA KUWASIFI MTUNZE MAZINGIRA. LAKINI HAYO YAMEPITA, YAJAYO NI KURUDISHA KIJANI MAKUTANO

KUNA NJIA NNE TUNAZOWEZA ANZA ZIFANYA KUOKOA MAZINGIRA YETU. MOJA NI KUANZA KUPANDA MITI SAHIHI KATIKA ENEO SAHIHI, KAMA VILE YA MATUNDA KAMA PARACHICHI KULE BONDENI.



PILI NI KUACHA KABISA KUKATA MITI KIHOLELA, KUCHOMA MKAA NA KUTUMIA NISHATI MBADALA KATIKA KUPIKIA NA MATUMIZI MENGINE, KAMA MIKAA YA KARATASI, MAJIKO YA UMEME NA GESI.

DUIH, MADOGO WANAAKILI KUMBE, WAMENITOA USHAMBA.



SALIMA ANAFANYA NINI TENA?

TATU NI KUPUNGUZA, KUCHAKATA TENA NA KURUDIA TUMIA BIDHAA HASA ZA PLASTIKI ILIKUPUNGUZA KUTUPA NA KUCHOMA TAKA, ZINAZOATHIRI MAZINGIRA YETU.

BILA KUSHIRIKIANA PAMOJA, MAKUTANO ITAPOTEZA KIJANI KABISA NA UOTO WAKE WA ASILI HAUTONEKANA TENA NA SISI WATOTO TUTABAKI NA MAVUMBI TU.

MMMH, MBONA KAMA ANAONGEA POINT.



SAFARI YA KUBADILIKA ILIANZA. KILA SIKU KWA MIEZI ISHIRI NA NNE WANAKIJIJI WALIFANYA USAFI.

MWALIMU YASINTA ALISHIRIKIANA NA WATAALAMU WA MIMBA NA UDONGO, KUWAFUNDISHA KINA SALIMA NA WANAKIJIJI MITI SAHIHI YA KUPANDA.



MIAKA MIWILI BAADAJE.

MMM!
NIMEKWISHA SINA CHANGU,
BINADAMU WAMEANZA SHIRIKIANA
KUTUNZA MAZINGIRA NA
KUPAMBANANA MABADILIKO
YA TABIA NCHI.

MAHUSIANO BAINA YA SALIMA NA BABA YAKE YALIIMARIKA NA WALISHIRIKIANA
KUJENGA KARAKANA NA BIASHARA YA UTENGENEZAJI SAMANI ZA VYUMA
IKAWA NJIA MPYA YA KUINGIZA PESA.

HEWA SAFI, MAJI MASAFI,
MOJI SAFI, KWELI
SALIMA WEWE NI MLINZI
WA DUNIA YA KIJANI.

SASA HIVI NAFURAHIA
KUISHI NDANI YA
KIJAJI CHETU.

AHSANTE BABA NA MAGUGU
AMEPOTEA KABISA.
NIFURAHA KUONA JUHUDI
ZA KUTUNZA
MAZINGIRA ZIKIONEKANA,
KESHO YETU NI YA
KIJANI.

MASWALI

1. JE SHULENI KWENU MNA KLABU YA MAZINGIRA? KAMA IPO TUELEZE HUWA MNAFANYA NINI? KAMA HAIPO, HUWA UNA JIFUNZA WAPI MASUALA YA MAZINGIRA?
2. TUAMBIE NI KITU GANI UMEJIFUNZA KUTOKA KWA SALIMA?
3. TUAMBIE NI KITU GANI UMEJIFUNZA KWA WATU WAZIMA KAMA MWALIMU YASINTA, BABA SALIMA NA BIBI SALIMA?



Walinda Mazingira, Salima na Amani, wameazimia kufanya mabadiliko katika mji wao wanaupenda kuishi na kusoma shule. Lakini wanakabiliwa na kishindo kikubwa: Magugu, mwovu mwenye tamaa ya kuwasahaulisha watu ubaya wa matumizi ya plastiki, kukata miti na uchafu unaoleta kuharibu mazingira!

Je! Salima na Amani watafanikiwa kuvunja vifungo vya giza vya Magugu na kufufua mazingira yao?

Jiunge na safari hii ya kusisimua ya ujasiri, urafiki na mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira!



We World SÜDWIND



Funded by the European Union

WAKUWA MATATA Tail

This publication was produced with the financial support of European Union. Its contents are the sole responsibility of WeWorld and do not reflect the views of the European Union